# MODULI YA KUTENGENEZA SABUNI

## HATUA YA KWANZA



## IPOSA

TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

# MPANGO WA ELIMU CHANGAMANI KWA VIJANA WALIO NJE YA SHULE

## MODULI YA KUTENGENEZA SABUNI

HATUA YA KWANZA

Kimeandaliwa na
Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
S.L. P. 20679
Dar es Salaam
**Tanzania**

Pepesi: +255 222 150836
Baruapepe: info@iae.ac.tz
Wavuti: www.iae.ac.tz

© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, 2019

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuchapa wala kudurufu Kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

## Shukurani

Shukurani za pekee ziwaendee wataalamu wafuatao kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu wzima, taasisi nyingine na watu binafsi kwa juhudi zao za pamoja katika kukamilisha uandishi wa moduli hii.

**Waandishi**

Dkt Sempeho I. Siafu — Taasisi ya elimu ya watu wazima
Wilfred wambura — SIDO, mororgoro

**Waratibu**

Leonia Kassamia — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
Dkt Sempeho I. Siafu — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

**Mshauri**

Dkt. Honest Kipasika — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

**Wahariri**

JohnBosco Mihigo — Mshauri wa uhariri UNICEF
Erick Samba — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

**Wachoraji**

Bakari Ngwawasya — Mstaafu Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
Mohamed L. Haruna — Mwalimu H/W Handeni Tanga
Haji R. Chamng'anda — Mchoraji huru, Morogoro

**Mpiga picha**

Leonard M. Lupeja — Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

**Wachapaji**

| | |
|---|---|
| Zena Rajabu Kazala | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |
| Neema Rumisha | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima |

..........................................................

Dkt. Michael W.Ng'umbi
Mkurugenzi Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima

# Yaliyomo


Kuhusu MODULI .................................................. vii
Muundo wa MODULI .......................................... vii
Maelezo ya jumla kuhusu moduli ...................... ix
**Somo la Kwanza** .................................................. 1
Matumizi ya Sabuni .......................................... 1
Soma .............................................................. 2
**Somo la Pili** .......................................................... 3
Aina za Sabuni .................................................. 3
Soma .............................................................. 4
**Somo la Tatu** ........................................................ 5
Kutengeneza Sabuni ........................................ 5
Unda maneno .................................................. 5
Soma .............................................................. 6
Hesabu ............................................................ 6
**Somo la Nne** ........................................................ 7
Faida za Sabuni ................................................ 7
Unda maneno .................................................. 7
Soma .............................................................. 8
Hesabu ............................................................ 8
**Somo la Tano** ...................................................... 9
Kuuza Sabuni .................................................. 9
Unda maneno au sentensi .............................. 10
Soma .............................................................. 10
Hesabu ............................................................ 10
Andika ............................................................ 10

**Somo la Sita** .......... 11
Kutunza Kumbukumbu za Mradi .......... 11
Unda maneno au sentensi .......... 12
Soma .......... 12
Hesabu .......... 12
Andika .......... 13
**Somo la Saba** .......... 14
Daftari la Kumbukumbu za Mapato na
Matumizi .......... 14
Soma .......... 14
Hesabu .......... 15
Andika .......... 15
**Somo la Nane** .......... 16
Herufi za Kiswahili .......... 16

## Kuhusu MODULI

Kutengeneza Sabuni Hatua ya Kwanza imetayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. MODULI zote zilizotayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima zina muundo sawa, kama ilivyoelezwa hapa chini.

## Muundo wa MODULI

Maelezo ya jumla kuhusu moduli

Maelezo haya yanatoa utangulizi kuhusu moduli hii. Habari zinazopatikana katika maelezo ya jumla kuhusu moduli zitakusaidia kuamua:

- Kama moduli hii inakufaa.
- Kile unachohitajika kukijua kabla ya moduli hii.
- Unachoweza kutarajia kutoka kwenye moduli.

Maelezo haya ya jumla pia hutoa mwongozo juu ya:

- Umahiri wa jumla,
- Mbinu za usomaji,
- Jinsi ya kupata usaidizi na
- Ishara za pambizo zinazotumika kwenye masomo

Tafadhali soma kwa makini maelezo ya jumla kuhusu moduli kabla ya kuanza masomo ya moduli hii.

## Yaliyomo kwenye moduli

Moduli hii imegawanywa katika masomo. Kila somo lina:

- Utangulizi.
- Matokeo ya kujifunza.
- Maudhui ya somo
- Tafakuri na
- Zoezi.

## Marejeleo

Kwa wale wanaopenda kujifunza mengi juu ya mada hii, tunawapa orodha ya marejeleo ya ziada mwishoni mwa MODULI hii; haya yanaweza kuwa vitabu, makala au tovuti.

## Maoni yako

Baada ya kukamilisha moduli ya Kutengeneza Sabuni tutashukuru ikiwa utatenga muda mfupi kutupa maoni yako kuhusu kipengele cho chote cha moduli hii. Maoni yako yanaweza kuhusu:

- Yaliyomo kwenye moduli na muundo wake.
- Makala za kusoma kwa moduli na marejeleo mengine.
- Mazoezi yaliyomo kwenye masomo ya moduli hii.
- Tathmini za moduli.
- Usaidizi katika moduli (walimu waliofundisha moduli, usaidizi wa kiufundi, n.k.)

Ukitoa maoni mwafaka utatusaidia kuboresha moduli hii.

## SOMO LA KWANZA

### Matumizi ya Sabuni





Sabuni hutumika kufulia, kuogea, kunawia na kuoshea.

Ondoa uchafu mwilini kwa kuoga na sabuni.

Zamani sabuni zilitumika kufulia, kuogea na kunyolea ndevu.

Endelea kutumia sabuni uepuke magonjwa.

Sabuni zilitengenezwa kwa mafuta ya mmea, wanyama na majivu.

Sasa hivi sabuni hutengenezwa kitaalamu zaidi na ina matumizi mengi.

sa-bu-ni i-na-tu-mi-ka ku-fu-li-a ku-o-ge -a

a u i o e

ku-na-wi -a ku-o-she-a

a e i o u:

## Soma

sabuni ya kufulia

sabuni ya kuogea

## SOMO LA PILI

### Aina za Sabuni






Zipo aina nne za sabuni.
sabuni ya mche,
sabuni ya unga,
sabuni ya maji na
sabuni maalumu.

u-nga ma-ji m-che

u a i e

ma-a-lu-mu sa-bu-ni

a e i o u

ma sa ni bu ji nga che lu

## Soma

Sabuni ya mche


Sabuni ya unga

Sabuni ya maji

Sabuni maalumu

## SOMO LA TATU

### Kutengeneza Sabuni



Sabuni hutengenezwa kwa kutumia mikono au mashine.
Tunatengeneza sabuni kwa matumizi ya nyumbani.
Tuzingatie kanuni za utengenezaji wa sabuni.
Tutengeneze sabuni, tuziuze ili tupate pesa.

ma-shi-ne     sa-bu-ni     pe-sa
u a e i
tu-pa-te     sa-bu-ni     tu-zi -u-ze   i-li
a e i o u
ma ne bu sa pe tu ze shi

### Unda maneno

pesa butu mama sasa bubu nesa zetu
tuma mashine

## Soma

mapema tabibu pasi kata
tazama mabati pasuka shati
patanisha nani nishati komesha

## Hesabu

Soma namba

1 2 3 4 5 6 7 8 9

sabuni mbili
2

sabuni tatu
3

sabuni nne
4

mashine tano
5

mashine sita
6

sabuni saba
7

mashine nane
8

mashine tisa
9

## Soma

mapema tabibu pasi kata
tazama mabati pasuka shati
patanisha nani nishati komesha

## Hesabu

Soma namba

1 2 3 4 5 6 7 8 9

| | | |
|---|---|---|
| sabuni mbili | sabuni tatu | sabuni nne |
| 2 | 3 | 4 |
| mashine tano | mashine sita | sabuni saba |
| 5 | 6 | 7 |
| mashine nane | mashine tisa | |
| 8 | 9 | |

## SOMO LA NNE

### Faida za Sabuni




Sabuni ina faida nyingi.

Sabuni hutusaidia kusafisha na kuondoa uchafu.

Sabuni ni dawa ya kuzuia na kuua viinimaradhi.

Sabuni hutumika kulainisha misumari kabla ya kutoboa.

sa-bu-ni da-wa u-cha-fu -ku-zu-i-a wa-du-du

a u i

a e i o u

sa ni da bu wa fu ku zu du
cha

**Unda maneno**

kuni chafu dafu kuku fuzu sawa dubu

sasa buni duni sanifu dada

## Soma

kuni chafu dafu kuku fuzu sawa dubu

sanifu dada

## Hesabu

Soma namba

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 10 | 20 | 30 | 40 | 50 | 60 | 70 | 80 | 90 | |
| 15 | 25 | 35 | 45 | 55 | 65 | 75 | 85 | 95 | 100 |

## SOMO LA TANO

### Kuuza Sabuni



Sabuni zilizotengenezwa vizuri hupata soko. Tuhifadhi sabuni vizuri ili zisiharibike. Tuuze sabuni ili tupate pesa.

sa-bu–ni zi-li–zo-te-nge-ne-zwa vi-zu-ri hu-pa-ta so-ko

a u i o e

a e i o u

| | | |
|---|---|---|
| ta te ti to tu | fa fe fi fo fu | ba be bi bo bu |
| ha he hi ho hu | sa se si so su | na ne ni no nu |
| va ve vi vo vu | pa pe pi po pu | ka ke ki ko ku |

ra re ri ro ru

nga nge ngi ngo ngu

zwa zwe zwi zwo zwu

dha dhe dhi dho dhu

## Unda maneno au sentensi

karatasi sare kata vuka tikisa patikana katazwa hataki shangazwa kadhalika tatizo pangusa dhahabu

Karatasi zinapatikana kabatini.

Tikisa kikapu.

Rafiki yangu kanipa pete

## Soma

Sabuni zilizotengenezwa vizuri hupata soko. Tuhifadhi sabuni vizuri ili zisiharibike. Tuuze sabuni tupate pesa

## Hesabu

Soma namba

| | | |
|---|---|---|
| 200 | - | mia mbili |
| 250 | - | mia mbili hamsini |
| 300 | - | mia tatu |
| 350 | - | mia tatu hamsini |
| 400 | - | mia nne |
| 450 | - | mia nne hamsin |

## Andika

Sabuni zilizotengenezwa vizuri hupata soko.

Tuhifadhi sabuni vizuri ili zisiharibike.

Tuuze sabuni tupate pesa

# SOMO LA SITA

## Kutunza Kumbukumbu za Mradi

Mtiririko wa Fedha Jan - Jun 2011 (Mfano)

| | Mwezi wa kwanza | Mwezi wa pili | Mwezi wa tatu | Mwezi wa nne | Mwezi wa tano |
|---|---|---|---|---|---|
| Kianzio | 20 | (90) | (70) | (10) | 40 |
| MAPATO | | | | | |
| Mauzo kwa fedha taslimu | 100 | 250 | 300 | 300 | 200 |
| Malipo toka kwa wadaiwa | 30 | 40 | 30 | 30 | 30 |
| Jumla ya fedha | 150 | 200 | 260 | 310 | 270 |
| MALIPO | | | | | |
| Manunuzi kwa fedha taslimu | 110 | 130 | 130 | 130 | 110 |
| Malipo kwa wadai | 40 | 40 | 40 | 40 | 40 |
| Mishahara | 30 | 30 | 30 | 30 | 30 |
| Ununuzi wa mafuta | 60 | 70 | 70 | 70 | 60 |
| Jumla ya malipo | 240 | 270 | 270 | 270 | 240 |
| Salio | (90) | (70) | (10) | (40) | 20 |
| (Pungufu) | | | | | |

Kumbukumbu huonesha shughuli za utengenezaji sabuni.

Tujue tarehe ya kununua malighafi.

Tujue tarehe ya kuanza kutengeneza sabuni.

Tujue tarehe ya kuanza kuuza sabuni.

Ni muhimu kutunza kumbukumbu za mradi.

mu-hi-mu ku-tu-nza ku-mbu-ku-mbu

ma me mi mo mu ka ke ki ko ku ta te ti to tu

za ze zi zo zu da de di do du ha he hi ho hu

nza nze nzi nzo nzu mba mbe mbi mbo mbu

## Unda maneno au sentensi

kiko zeze keki matatizo hekima haki kamba meza
kikombe kanzu nzito dakika mbata

Weka kumbukumbu za mapato.

Matumizi ya kutengeneza sabuni yasizidi mapato

## Soma

Kumbukumbu huonesha shughuli za utengenezaji wa sabuni.

Tujue tarehe ya kununua malighafi.

Tujue tarehe ya kuanza kutengeneza sabuni.

Tujue tarehe ya kuanza kuuza sabuni.

Ni muhimu kutunza kumbukumbu za mradi

## Hesabu

Kujumlisha (+) na kutoa (-)

| | | | |
|---|---|---|---|
| 250 | 550 | 450 | 900 |
| + 200 | + 400 | - 240 | - 600 |
| ______ | ______ | ______ | ______ |

## Andika

Tuweke kumbukumbu za mradi wetu. Zitasaidia kuonesha hali halisi ya biashara. Tutajua kama kuna faida au hasara.

Mfano wa jedwali la Utengenezaji wa Sabuni

| Tarehe | Kazi zilizofanyika |
| --- | --- |
| 6.3.2017 | Kununua malighafi (kemikali, rangi, kalibu) |
| 10.3.2017 | Kuanza kutengeneza sabuni |
| 24.3.2017 | Kuanza kuweka sabuni katika vifungashio |
| 3.4.2017 | Kuanza kuuza sabuni |

## SOMO LA SABA

### Daftari la Kumbukumbu za Mapato na Matumizi

| Mapato | | | Matumizi | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Tarehe | Maelezo | Kiasi cha fedha | Tarehe | Maelezo | Kiasi cha fedha |
| 15.2.2017 | Msaada toka kwa wanakijiji | Sh. 40,000/= | 6.3.2017 | Kununua malighafi | Sh. 170,000 |
| 26.3.2017 | Toka mfuko wa mbunge | Sh. 300,000/= | 10.3.2017 | Kununua vifaa | Sh. 30,000/= |
| 4.4.2017 | Mauzo ya bidhaa | Sh. 350,000/= | | | |

Daftari hutunza kumbukumbu za mapato na matumizi ya mradi.

Huonyesha mapato na matumizi.

Tuandike kumbukumbu za mradi katika daftari.

hu-o-ne-sha ma-pa-to na ma-tu-mi-zi

| | |
|---|---|
| ha he hi ho hu | pa pe pi po pu |
| ma me mi mo mu | na ne ni no nu |
| ta te ti to tu | za ze zi zo zu |
| nya nye nyi nyo nyu | sha she shi sho shu |

### Soma

Daftari la kumbukumbu ni muhimu katika kuendeleza mradi. Linatunza kumbukumbu muhimu za biashara. Tutumie daftari hilo kupata mafanikio.

## Hesabu

Matumizi ya mradi ni shilingi 590

Mauzo ya sabuni ni shilingi 990

Faida ya mradi ni shilingi 400

| | | | |
|---|---|---|---|
| 750 | 650 | 500 | 600 |
| - 200 | - 300 | - 240 | - 100 |
| ____ | ____ | ____ | ____ |

## Andika

Daftari la kumbukumbu ni muhimu katika kuendeleza mradi. Linatunza kumbukumbu muhimu za biashara. Tutumie daftari hilo kupata mafanikio.

Mfano wa Daftari la Mapato na Matumizi

| **Mapato** | | | **Matumizi** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Tarehe | Maelezo | Kiasi cha fedha | Tarehe | Maelezo | Kiasi cha fedha |
| 15.2.2017 | Msaada toka kwa wanakijiji | Sh. 40,000/= | 6.3.2017 | Kununua malighafi na vifaa (kemikali, rangi, kalibu, vifungashio) | Sh. 170,000 |
| 26.3.2017 | Toka Mfuko wa Mbunge | Sh. 300,000/= | 10.3.2017 | Kununua rangi | Sh. 30,000 |
| 4.4.2017 | Mauzo ya sabuni | Sh. 350,000/= | | | |

## SOMO LA NANE

### Herufi za Kiswahili

Kwa wakati huu umesoma herufi karibu zote za Kiswahili

| | | |
|---|---|---|
| a | Aina | Aina |
| b | Bibi | Bibi |
| c | - | - |
| d | Dakika | Dakika |
| e | endelea | Endelea |
| f | Faida | Faida |
| g | gawana | Gawana |
| h | Hataki | Hataki |
| i | inatumika | Inatumika |
| j | Jamani | Jamani |
| k | Kufulia | Kufulia |
| l | Lima | Lima |
| m | Maji | Maji |
| n | Nani | Nani |
| o | Ondoa | Ondoa |
| p | Pesa | Pesa |
| r | Rafiki | Rafiki |
| s | Sabuni | Sabuni |
| t | Tazama | Tazama |
| u | Unga | Unga |
| v | Vizuri | Vizuri |
| w | Wezesha | Wezesha |
| y | Yake | Yake |
| z | Zake | Zake |

Herufi nyingine

| | |
|---|---|
| ch | chama |
| sh | shaka |
| ng | Ngoja |
| dh | Dhahabu |
| mb | Mbata |
| ny | Nyanya |
| ch | Mche |
| nd | - |
| ng | zilitengenezwa |
| nz | Kutunza |

Printed By: Institute of Adult Education
S.L.P 20679, Dar es Salaam, Tanzania
Tel:+255 22 2150838, Fax: +255 22 2150836
Website:www.iae.tz Email:info@iae.ac.tz